**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2014**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18).**
2. Jibu Maswali yote katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na kila sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30).**
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhiswa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (ALAMA 40)

Jibu maswali **yote**

1. Taja mambo manne (4) ya kuzingatia katika kukuza stadi za kuzungumza na kusikiliza.
2. Bainisha manufaaa manne ya kutumia onesho mbinu katika kujifunza somo la Kiswahili.
3. Taja sifa nne za ushairi wa nyimbo.
4. (a) Elezea tofauti iliyopo baina ya njia ya kufundishia na mbinu ya kufundishia.

   (b) Bainisha kwa kifupi tofauti iliyopo kati ya mtaala na muhtasari wa somo la Kiswahili.
5. Taja mambo manne ya kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti.
6. Andika nomino moja kwa kila neno lifuatalo:
   (a) Lia
   (b) Piga
   (c) Choma
   (d) Kata
7. Elezea kwa kifupi hatua nne za kufuta wakati wa kufundisha imla.
8. Fafanua kwa kifupi tofauti iliyopo kati ya shajara na andalio la somo.
9. Elezea kwa kifupi tofauti iliyopo baina ya zana za kufundishia na za kujifunzia.
10. Ainisha aina nne za tungo katika lugha ya Kiswahili.

## SEHEMU B (ALAMA 30)

Jibu maswali **mawili (02)**

11. Elezea aina ya mazoezi anayoweza kupewa mwanafunzi ili kukuza stadi ya kuzungumza.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

12. Fafanua matendo manne yanayodhihirisha ufahamu kwa mwanafunzi baada ya kusoma habari.
13. Bainisha na elezea tofauti zilizopo kati ya barua ya kikazi na barua ya magazetini.
14. (a) Elezea maana ya vitendawili,
    (b) Elezea kwa mifano sababu sita za kufundisha wanafunzi somo la vitendawili.

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

Jibu maswali **mawili (02)**

15. Fafanua sifa tano za zana za kufundishia.
16. Toa mifano kubainisha manufaa matano anayopata mwalimu kwa kutoa majaribio na mitihani kwa mwanafunzi wake darasani.
17. Elezea mbinu tano ambazo mwalimu anaweza kutumia katika ufundishaji.
18. Elezea mapungufu matano ya kutumia mbinu ya ziara katika kufundisha somo la Kiswahili.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org